# Misingi Jamii ya Kitaaluma katika Ustaarabu

# MTAZAMO WA MALIK BENNABI

Badrane Benlahcene



Misingi Jamii ya Kitaaluma katika Ustaarabu
MTAZAMO WA MALIK BENNABI

Mfasiri: Hassan Mohamed

THE INTERNATIONAL INSTITUTE OF ISLAMIC THOUGHT

IIIT — Mfululizo wa Vitabu kwa Muhtasari

# *Misingi Jamii ya Kitaaluma katika Ustaarabu*

# MTAZAMO WA MALIK BENNABI

**SWAHILI VERSION**

Idara ya Lugha na Ukalimani ya Chuo Kikuu
cha Waislamu cha Morogoro

©International Institute of Islamic Thought, 2003

International Institute of Islamic Thought (IIIT)
P.O.Box 669
Herndon, VA 20172, USA
www.iiit.org
16 / 03/ 1429 AH 24/ 03/ 2008 AD

Hakimiliki ya Kitabu hiki imehifadhiwa. Hairuhusiwi kukipiga chapa, kwa namna yoyote ile bila ruhusa ya maandishi ya wachapaji.

Rai na maoni yaliyo elezwa katika kitabu hiki ni ya mwandishi, na si lazima yatangamane na yale ya wachapaji.

Kimetafsiriwa na:

Hassan Mohamed

Kimehaririwa na:

Hadija Kutwa Abdallah

Design and layout by:

Iddi Suleiman Kikong'ona (iddkiko@ymail.com)

# MFULULIZO WA MUHTASARI WA VITABU VYA IIIT

Mfululizo wa muhtasari wa Vitabu vya IIIT[1] ni hazina muhimu sana katika machapisho ya taasisi hii vilivyoandikwa kwa ufupi kabisa ili kumwezesha msomaji kuelewa dhamira kuu ya kitabu asilia. Vitabu vimeandikwa kwa ufupi ili kusomeka kwa urahisi na kuokoa muda hasa kwa waliotingwa na kazi. Machapisho haya yanatoa mwongozo wa dhima kuu, hivyo kumfanya msomaji kuwa na ari ya kutafuta nakala ya kitabu chenyewe.

***Misingi Jamii ya Kitaaluma Katika Ustaarabu : Mtazamo wa Malik Bennabi*** kilichapishwa mwaka 2011. Tangu insha ya Huntington "Mgongano wa Ustaarabu", kwa mara ya kwanza ilipozungumzia ustaarabu na mgogoro uliporudishwa katika mjadala duniani kote. Malik Bennabi aliyezaliwa mwaka 1905 na kufariki 1973 alikuwa si tu msomi maarufu wa Ki-Aljeria lakini pia mwanazuoni wa Kiislamu aliyebobea katika kutafiti anguko la Ustaarabu wa Kiislamu na mafanikio ya Ustaarabu na Utamaduni wa Kimagharibi. Tatizo kubwa alililoliona Bennabi halina msingi katika Qur'an au imani ya Kiislamu lakini kwa Waislamu wenyewe. Mwandishi huyu anachunguza mbinu ya Bennabi kuelekea ustaarabu na pamoja na misingi yake mikuu kwa kutumia nadharia mtambuka. Kwa kufanya hivi, anatoa mwanga zaidi katika moja ya sifa za nadharia ya Bennabi inayosema Ustaarabu unasimamiwa na sifa

1. Ni ufupisho wa *International Institute of Islamic Thought* iliyo tafsiriwa kwa Kiswahili kama Taasisi ya Kimataifa ya Fikra ya Kiislamu

za Misingi jamii ya kitaaluma ya ndani na nje na kwamba mlingano unaweza kutokana na ustaarabu wenyewe. Yaani Mtu+Ardhi+Muda= Ustaarabu ambapo kwa mujibu wa Bennabi, dini ina nafasi kubwa na umuhimu mkubwa katika harakati za kuokoa anguko la Uislamu. Kimsingi Bennabi anaamini kuwa mtu ni nguvu msingi katika hatua za kuelekea ustaarabu na kwamba bila yeye misingi mingine haiwezi kuwa na thamani.

Katika kutathmini matokeo ya nadharia ya Bennabi kwamba kama Waislamu hawatabadilika kiimani hawawezi kufikia malengo ya kuleta mabadiliko chanya katika jamii kama ilivyobainishwa katika Qur'ani tukufu

> *"Hakika Mwenyezi Mungu hatabadilisha hali za watu mpaka wao wabadilike" (13:11).*

Chapa iliyohaririwa kutoka kazi halisi ya Badrane Benlahcene

Mtazamo wa Misingi jamii ya Kitaaluma wa Malik Bennabi katika Ustaarabu

ISBN hbk: 978-1-56564-368-0

ISBN pbk: 978-1-56564-367-3

2011

## Yaliyomo

**NENO LA AWALI**
*Mfululizo Wa Muhtasari Wa Vitabu Vya IIIT...v*

**UTANGULIZI**
*1*

**SURA YA KWANZA**
*Ustaarabu: Dhana na Mitazamo* 5

**SURA YA PILI**
*Dhana Kuu za Bennabi Katika Ustaarabu* 9

**SURA YA TATU**
*Tafsiri ya Harakati za Ustaarabu* 13

**SURA YA NNE**
*Kigezo cha Ndani cha Kijamii* 20

**SURA YA TANO**
*Kigezo cha Nje cha Kijamii* 24

**SURA YA SITA**
*Kigezo cha Ndani cha Kitaaluma* 27

**SURA YA SABA**
*Kigezo cha Nje cha Kitaaluma* 30

# UTANGULIZI

Kitabu hiki kinajikita katika kazi ya Malik Bennabi (1905-1973), msomi maarufu wa Ki-Aljeria na mwanazuoni nguli wa Kiislamu aliyeleta mbinu na falsafa mpya. Kazi ya Bennabi ambayo imechanganua kwa kina sababu za kudhoofika kwa Uislamu na kustawi kwa Ustaarabu na utamaduni wa Kimagharibi inahitimisha kuwa matatizo hayako katika Qur'an au imani ya Kiislamu bali kwa Waislamu wenyewe. Picha halisi ya madhara ya ukoloni na sababu zinazolinda ustaarabu zingeweza kutatua matatizo ya ulimwengu wa Kiislamu na kusimamisha zama mpya ya ustawi wa Uislamu.

Kazi hii inachanganua mtazamo wa Bennabi katika ustaarabu na misingi inayotokana na nadharia mtambuka, yaani kwenda zaidi ya rejea zilizopo kuwasilisha mtazamo huu mtambuka wa Bennabi kuelekea ustaarabu na kuchambua muundo wake. Hii ni kusema kwamba kazi hii inamulika nadharia ya Bennabi kwamba sababu za ndani na nje za Misingi Jamii ya Kitaaluma zinabeba ustaarabu na kwamba mlingano unaweza kutoka katika ustaarabu wenyewe.

Kwa mujibu wa Bennabi, dini ndio kichocheo muhimu zaidi katika mlingano huu wa Mtu + Ardhi + Muda = Utaarabu na ni muhimu pia katika kuurudisha ustawi wa Uislamu duniani. Bennabi anaona Mtu ni msingi mkuu wa ustaarabu na kwamba bila yeye misingi mingine haina maana.

Imani ya Bennabi kwamba Waislamu lazima wabadilishe kwanza imani zao kabla ya kufanikisha mabadiliko katika jamii au ustaarabu kama ilivyobainishwa katika Qur'an tukufu (13:11)

> *"Hakika Allah habadilishi hali za watu mpaka wao wabadilike."*

Utafiti juu ya ustaarabu na mabadiliko ya ulimwengu umeendelea kuwa gumzo kwa wasomi wengi. Watafiti wengi na wasomi wameshauri kudurusu kazi mbalimbali za wasomi wa ustaarabu. Bennabi ambaye ni mwananfalsafa wa Sayansi ya Jamii wa kwanza duniani baada ya Ibn Khaldun, kutafiti kuhusu sheria na misingi mikuu inayoongoza jamii na ustaarabu duniani kote na kutazama muelekeo na historia zake. Kujikita kwake katika kudhoofika kwa ustaarabu wa Kiislamu kumefanya Bennabi kutathmini kwa kina na kutoa suluhisho. Bennabi haishii tu katika sintofahamu katika uchumi, siasa na ilani lakini amesisitiza kazi za kifikra kama chachu ya maendeleo ya ustaarabu.

Kutokana na uelewa mkubwa juu ya Uislamu na Sayansi za jamii, Bennabi anachambua ufanisi wa jamii ya kibinadamu na tofauti za kitamaduni pamoja na ustaarabu katika mtazamo wa kiulimwengu. Amelenga kutatua matatizo ya kijamii kwa mwongozo wa ustaarabu, kigezo muhimu katika kuelewa mambo ya jamii na kihistoria. Bennabi amebainisha kuwa "Tatizo la kila mtu, kimsingi, ni lile litokanalo na ustaarabu."

Falsafa ya Bennabi ni mfumo mtambuka wa utambuzi wa mambo kwa uelewa wa kina wa Uislamu. Msimamo wake katika ustaarabu na misingi yake katika historia inasaidia kupima migogoro ya ustaarabu wa Uislamu na kuelezea vyanzo vyake pamoja na kutoa suluhisho. Mafunzo yake kisayansi pamoja na mtazamo wa kihistoria, kisosholojia na kifilosofia yamempa msingi mkubwa wa kuutathmini ustaarabu wa Ulaya na kuja na fikra halisi za uimara na udhaifu wa Umma wa Kiislamu.

Kazi hii inalenga kutazama sababu mbalimbali za mtazamo wa Bennabi juu ya ustaarabu kwa kutazama mbinu, mitazamo, nadharia na kutathmini hatua za mbinu zake. Kimsingi, lengo la kazi hii ni kuelewa ustaarabu wa kisasa na matokeo yake katika maisha ya kijamii na kutoa mwongozo wa kistaarabu kwa wafanya maamuzi.

Mbinu mtambuka ya Bennabi inatoa taswira ya juhudi za kisomi za ulimwengu wa Kiislamu tangu mapema karne ya 19 zilizolenga kutatua matatizo ya Waislamu na kuuinua ustaarabu wa Uislamu kupitia mfumo mpana wa tathmini. Matokeo yake yanatokana na falsafa ya kihistoria, sayansi jamii na urithi wa Ibn Khaldun. Mtazamo huu ni muhimu katika kupima sintofahamu mbalimbali katika ulimwengu wa Kiislamu na ustaarabu mwingine.

Tunatambua fikra za ustaarabu za Bennabi, kwa kutumia mtazamo huu wa nadharia mtambuka, ambayo kimsingi ni mfumo maalumu wa muundo wa nadharia ya kisosholojia. Mtazamo huu unanasibiana na muongozo wa kitaaluma ambao ni msingi mkuu wa maendeleo wa fikra za Bennabi. Mwandishi anatumia aina ya kwanza ya nadharia mtambuka . Shabaha ya utafiti huu ni kupata uelewa kuntu wa nadharia ya ustaarabu ya Bennabi pamoja na vigezo vinne vya nadharia ya mtambuka .

Nadharia mtambuka inajumuisha utafiti wa nadharia kupata uelewa wa kina wa nadharia iliyopo. Katika kutazama vigezo vya ndani vya kijamii, mbinu hii inaangazia ndani ya eneo la utafiti ambayo inajikita zaidi katika vigezo vya kijamii kuliko vya utambuzi. Kwa upande wa vigezo vya nje vya jamii, vyenyewe vinavuka mipaka hadi kufikia kiwango cha juu kwa kuitazama jamii kubwa na matokeo yake katika matumizi ya nadharia, wakati ikisisitiza uhusiano baina ya utaratibu wa upatikanaji wa nadharia na taasisi mbalimbali. Bennabi anaona kigezo hiki kinajikita katika uhusiano baina ya vigezo vya nje vya kijamii na uandaaji na maendeleo ya mtazamo huu.

Vigezo vya ndani vya kitaaluma vinaangazia taaluma au mambo ya utambuzi ambayo awali yalikuwa katika kigezo cha ndani katika ustaarabu. Hii inajumuisha jitihada za kutambua nadharia, mitazamo, mabadiliko ya nadharia pamoja na zana za nadharia mtambuka. Vigezo vya nje vya kitaaluma vyenyewe vinageukia nyanja nyingine za kitaaluma kwa ajili ya kupata mawazo, zana, fikra na nadharia mbalimbali kuelekea ustaarabu. Kwa mtazamo wa Bennabi, kigezo hiki kinajumuisha matokeo ya Qur'an, fikra za kidini katika ulimwengu wa Kiislamu, falsafa, saikolojia, sayansi asilia, pamoja na shughuli mbalimbali za kitaaluma nje ya uga wa elimu ya ustaarabu na nadharia zake mbili zilizozoeleka.

Nadharia mtambuka inatoa mbinu maalum za kupata uelewa, tathmini, ukosoaji na kuboresha nadharia zilizopo. Wanazuoni wa nadharia mtambuka wamefuatilia kwa kina, ulinganifu na uwanda mpana wa nadharia za kisosholojia. Kimsingi nadharia mtambuka, ina fursa kubwa kwa kufanya uchambuzi na tathmini ya kina kwa nadharia zilizopo.

Mbinu ya ulinganisho, inayotumiwa na utafiti huu, inatumia muundo wa nadharia mtambuka katika kuelewa mtazamo wa Bennabi na kulinganisha mtazamo huo na ule wa Ibn Khaldun na wengine. Utafiti huu unatumia mbinu mseto kwa kujumuisha tathmini ya kihistoria, tathmini ya ulinganisho na tathmini ya maudhui. Kwa mbinu hii ya kulinganisha, mwanandishi anakusudia kuelewa na kugundua kutofautiana na kufanana kati ya mtazamo wa Bennabi na mitazamo ya wanazuoni wengine. Mbinu ya tathmini ya kimaudhui inaonesha fikra, mitazamo na uelewa wa maelezo ya Bennabi, kufafanua muundo mkuu wa mtazamo wake, pamoja na mawazo mbalimbali kama mfumo katika uelewa wa kina kwa kuzingatia nadharia mtambuka. Kupiga hatua toka ufahamu mdogo hadi mkubwa ni kipimo kimojawapo cha ufahamu wa kifalsafa katika kushughulikia masuala tanzu katika jamii.

Vyanzo vikuu vya utafiti wa sasa, kufanyia tathmini mfumo na mtazamo wa Bennabi kuelekea ustaarabu ni kazi halisi ya Bennabi aliyechapisha kazi zake zote katika mada moja iitwayo Mushkilat al-Hadarah (matatizo ya ustaarabu), pamoja na kazi nyingine katika uga wa sosholojia na matawi yake mbalimbali kama vile: falsafa ya historia, anthropolojia, historia na nyinginezo. Mwanadishi anatumia vitabu vingine kama vyanzo vyake vya pili.

# SURA YA KWANZA

## *Ustaarabu: Dhana na Mitazamo*



Mtazamo mtambuka una mafanikio makubwa katika nadharia na utafiti katika ustaarabu kwa kuwa inajumuisha nyanja zote. Unapofanya utafiti kuhusu maendeleo ya dhana ya "ustaarabu" na mitazamo mbalimbali katika mambo yake katika kipindi chote cha historia, inaweza kusaidia utambuzi wa mitazamo mikuu katika uga wa utafiti katika mambo ya ustaarabu.

Kutambua namna gani dhana ya ustaarabu imemea kutoka katika utamaduni na lugha tofauti tofauti katika ustaarabu kuna changamoto kubwa hasa ulimwengu wa Kimagharibi na ule ufuatao utamaduni wa Kiislamu. Ugumu mwingine ni tofauti katika maana ya ustaarabu katika nyanja tofauti. Watafiti wengi wanakubaliana kuwa ustaarabu ni mjumuiko mpana kabisa wa tamaduni mbalimbali. Huntington, kwa upande wake anauweka ustaarabu katika uga wa kihistoria na maendeleo kwa kuzingatia muda. Pia anaunganisha ustaarabu na dini, sifa ya msingi ya ustaarabu kama alivyofanya Ibn Khaldun, Toynbee, Bennabi na wanazuoni wengine wa ustaarabu.

Uislamu na Mtume Muhammad (S.A.W), umebadilisha misingi ya mahusiano ya kijamii katika jamii za makabila ya Kiarabu mpaka katika misingi inayoegemea mawazo ya utamaduni wa kiraia wa Kiislamu pamoja na tofauti ya matabaka katika jamii na makundi ya kikabila. Kama muanzilishi wa jamii mpya na ustaarabu, Mtume Muhammad

(S.A.W) alitambua kuwa maendeleo ya maeneo ya mjini lazima yawe mbadala wa maisha ya kuhamahama na utamaduni wa kimakabila. Mji wake wa Madinah ulikuwa kitovu cha mabadiliko hayo ya ustaarabu.

Neno 'ustaarabu' lilitokea kwa mara ya kwanza katika utamaduni wa Kiislamu katika karne ya 14 katika maandiko ya Ibn Khaldun. Ibn Khaldun ndiye aliyetambulisha kwa mara ya kwanza hadarah na 'umran inayoweza kulinganishwa na neno 'ustaarabu' na 'Ilm al-'Umran (sayansi ya ustaarabu). Ibn Khaldun aliutazama ustaarabu kama taifa muhimu ambalo binadamu wanaishi pamoja. Dhana yake inaainisha sifa ya kubadilika katika hatua za maendeleo ya mwanadamu.

Dhana ya ustaarabu iliendelea zaidi miongoni mwa wanazuoni wa Kiislamu mwishoni mwa karne ya 19 pale Uislamu ulipopata nguvu na kupambana na Ulaya ya kisasa. Dhana ya hadarah ikawa maarufu katika majukwaa ya kisayansi na kisomi katika ulimwengu wa Kiarabu na Bennabi alikuwa mwanzilishi katika kuchagua kufafanua neno 'ustaarabu'. Katika lugha nyingine zitumikazo katika ulimwengu wa Kiislamu, madaniyyah au nyingine zinazofanana nazo zilitumika.

Mitazamo ya Kiislamu na ile ya Kimagharibi inakubaliana katika misingi mikuu ya ustaarabu kama; maisha ya mjini, mpango au taasisi, na maisha ya starehe. Maneno mbalimbali katika lugha tofauti yamekuwa yakitumika kufafanua dhana ya ustaarabu kwamba ustaarabu unajumuisha; jamii ya mjini, wengine toka serikalini, namna ya kisomi, uwezo wa watu kubadili mazingira yao na maisha yao, majukumu maalum, mtandao wa mahusiano ya jamii, na mfumo wa imani na dhana ya Mungu au nguvu nyingine.



Ingawa makubaliano katika sifa za msingi za ustaarabu, bado kuna mitazamo tofauti, mbinu tofauti, shabaha tofauti na dhana tofauti. Mitazamo mbalimbali inaonekana katika mirengo mikuu ya kifalsafa, historia, na sayansi jamii pamoja na mirengo midogo ya anthropolojia na sosholojia. Wasilisho hili linaonesha mfumo wa uelewa wa mambo ya ustaarabu kwa ujumla wake na kipekee katika dhana ya Bennabi.

Falsafa ya historia imeibuka kama jitihada za ufafanuzi wa mambo kwa mpangilio. Wakati historia ni muongozo wa kwanza, yaani stadi ihusuyo vitendo, matukio yaliyopita pamoja na hali ilivyo, na falsafa ya historia ni muongozo wa pili unaojumuisha stadi kuhusu mada husika. Inaweza kufahamika kuwa stadi mtambuka, ambayo hailengi moja kwa

moja, katika matukio, vitendo na hali tofauti tofauti, badala yake, stadi hii isiyo ya moja kwa moja inatafuta kuelezea na kufafanua majibu kuhusu mabo yaliyopita. Wanafalsafa wa historia wanatumia mitazamo mipana kuhusu michakato ya kihistoria.

Wanahistoria wanajaribu kuelezea mambo yaliyopita, sababu za kubadilika kwa jamii na mifumo ya kidunia katika mijongeo ya kihistoria. Baadhi ya kambi za kifalsafa zinasisitiza uwepo wa utashi wa kiungu wakati wengine wakiona ni jukumu la kila mtu, au uchumi na sababu zingine zimhusuzo mtu mmoja mmoja ndizo hufanya mchakato wa kihistoria. Katika mtazamo endelevu wa kihistoria, Plato, Herder, Hegel na wanazuoni wengine wa Ulaya wanaona mfumo wa Kiyahudi-Kikristo katika masuala ya muda na historia kama mchakato ulio katika mstari mnyoofu unaounganishwa na fikra za kisasa katika mizunguko ya kihistoria.

Bila kuwa na dhana inayokubalika kwa ujumla inayoweza kutoa mfumo wa umoja, waliojaribu kuandika historia ya ulimwengu wametumia mitazamo mitatu; muundo wa mfululizo wa utamaduni au ustaarabu ambao tamaduni zote zinafuata mfumo wa maendeleo; mfumo endelevu; na mfumo sambamba uliorahisi katika historia ya mwanadamu kwa kuzingatia watu mbalimbali. Mfumo wa mfululizo ndio mfumo ulioendelezwa sana na kujitokeza kutoka katika kazi za wasomi wakubwa wa ustaarabu kama Ibn Khaldun.

Ikilinganishwa na mfumo wa zamani wa falsafa ya historia na mitazamo mbalimbali ihusuyo ustaarabu, mtazamo ya sayansi ya jamii ndio kwanza unajitokeza. Anthropolojia ndio ilikuwa sayansi jamii ya mwanzo kugusa stadi ya ustaarabu wa binadamu na utamaduni wake. Ustaarabu katika mtazamo wa ki-anthropolojia, ni kiwango cha juu cha utamaduni na kitambulisho cha utamaduni.

Wataalamu wa sayansi ya jamii huisoma historia kwa njia tafauti. Njia ya sayansi ya jamii kihistoria haikusudii kuanza kujenga vigezo vya maendeleo vya mchakato wa mabadiliko uliosukwa kabisa. Badala yake, njia hii inajikita katika kutazama historia, ikichambua vipengele vya matukio ya kihistoria yaliyotuka kijamii, kwa kubaini vyanzo, sababu, na au nguzo zake. Kwa muktadha huu, ustaarabu kwa maana ya mchakato kabambe wa kihistoria na maendeleo unaokuwa kwa muda mrefu hatua kwa hatua, unahusisha upeo mkubwa wa sayansi ya jamii.

Kama ilivyo kwa wanafalsafa na wasomi wa historia, kadhalika watafiti wa sayansi pevu ya jamii wanaamini kuwa katika kitambo kirefu cha muhula wa kufanya uchambuzi, wanaweza kubaini kiini cha sababu za mabadiliko katika maisha ya mwanadamu.

Matatizo makuu katika wakati wa sasa yanaonekana kuongezeka kuwa ya ki-sosholojia kuu na hivyo kuhitaji nadharia ya inayokidhi uwanda huo na masuluhisho ya kiutafiti. Matatizo mengi ya sosholojia kuu (macrosociology) na maendeleo yake hayawezi kufahamika au kufanyiwa kazi isipokuwa katika muktadha mpana wa mambo ya kijamii. Sosholojia kuu na msisitizo wake katika uchambuzi wa vipengele mbalimbali imechangia kwa kiasi kikubwa katika stadi pana ya mambo kwa kutathmini michakato ya muda mrefu, mifumo ya kitamaduni, jamii na ustaarabu.

Sosholojia ya mabadiliko imechangia katika stadi ya ustaarabu na mabadiliko ya kihistoria kwa kutenganisha viwango vya mabadiliko kwa kuzingatia vigezo vya: ukubwa (familia, jamii, utamaduni, ustaarabu, ulimwengu); muda (wa kihistoria, kipindi kirefu, kipindi kifupi; au kigezo cha nyanja zenyewe (ya kitamaduni, ya kisomi, na ya kistaarabu).

Mtazamo wa sayansi jamii unajikita katika ushahidi unaoonekana umekwepa maswali mengi ya nadharia na falsafa. Ushahidi umeainisha mahitaji ya ki-mbinu katika stadi mtambuka na tathmini ya hatua kwa hatua katika upana wake. Dhana nyingi za 'ustaarabu' zingeweza kusaidia kuzingatia sifa za sura tofauti tofauti na mitazamo iliyopo isiyotosha. Kushindwa kwa mitazamo mingine kusimamia ufahamu juu ya stadi za ustaarabu kunaona ustaarabu hauwezi kutoshelezwa sawasawa katika ngazi zote katika kutenganisha mambo, bali yanapaswa kujumuishwa katika muktadha wa mtazamo wa kiulimwengu.

# SURA YA PILI

## *Dhana Kuu za Bennabi Katika Ustaarabu*



Bennabi alikosoa nyendo za wana-mabadiliko na wana-usasa katika ulimwengu wa kisasa wa Kiislamu kwa kushindwa kubainisha sababu za migogoro na kujikita katika dalili tu. Bennabi anaeleza kwamba juhudi za kuanzisha zama za muamko katika ulimwengu wa Kiislamu hazikuweka misingi inayofuata hatua maalumu kupambana na migogoro. Tatizo limeanzia katika utamaduni wa kiislamu baada ya kipindi cha al-Muwahhid na Bennabi alisema mchakato wa kihistoria ulifungua njia kutokea kwa ukoloni. Kujitokeza kwa ukoloni si sababu kubwa hata hivyo kwa hali ya sasa ya ulimwengu wa Kiislamu, lakini ni urahisi wetu wa kutawalika katika sababu nyingi za kuongezea.

Ufafanuzi wa Bennabi kuhusu ustaarabu unatofautiana. Alitambua kwamba ustaarabu unawezesha uwezo wa kijamii kupambana na matatizo makubwa katika jamii, na kuonesha mizania kati ya nyanja ya kimaadili na nyanja ya kidunia katika maisha ya mwanadamu. Kwa kuwa jamii inathibitisha shughuli za kibinadamu katika utawala wa historia, jamii inakuwa ni nguvu ya msingi katika mchakato wa ustaarabu.

Bennabi alifafanua kuwa nyanja za kimaadili na kimaada ni muhimu katika kutengeneza mizania na usawa katika jamii ya kibinadamu na hivyo kudumisha umoja na mshikamano. Akiielezea dhana ya

ustaarabu kwa kutumia muundo wake na mantiki yake ya kijamii, Bennabi anasema, ustaarabu ni: "…mwanadamu anajifunza namna ya kuishi katika kikundi na anaelewa…umuhimu mkuu wa mtandao wa mahusiano ya kijamii katika kupangilia maisha ya binadamu kwa ajili ya kutekeleza kazi na majukumu ya kihistoria."

Kwa Bennabi, kanuni ya "Ustaarabu = Mtu + Ardhi + Wakati" unawakilisha mlinganyo wa ustaarabu, ambao kimuundo unafanya sifa au viungo vyake. Sifa hizi za msingi za aina yoyote ya vitendo vya kistaarabu au zao inaonesha kwamba matatizo ya ustaarabu yanafanya mgawanyiko katika makundi makuu matatu: Mtu, ardhi na wakati.

Bennabi anaeleza kuwa vitu vyote anayotengeneza binadamu vinatokana na mtu (Insan), ardhi (Turab), na wakati (Waqt). Vitu hivi vitatu vinavyopatikana katika kila jamii ni msingi mkuu kwa jamii kuanza mchakato wa ustaarabu. Tunapozungumzia kisayansi, uundaji wa tabia za mtu, matumizi ya ardhi, na mpangilio wa wakati, ndio muda maalumu ambao ustaarabu unatoa huduma muhimu kwa jamii pamoja na msaada katika mahitaji ya binadamu kwa ajili ya maendeleo. Katika mlinganyo huu, mtu (Insan), ni zana ya msingi ya ustaarabu na nguvu ya msingi katika mchakato wa ustaarabu. Bennabi anapingana na harakati za wana-mageuzi katika ulimwengu wa Kiislamu katika kubadilisha mazingira yake kuliko sababu za kibinadamu, na kuhoji kwamba tunapaswa kumbadilisha mwanadamu. Bennabi anaeleza kwamba ustaarabu unakuwa kutokana na mwanadamu mwenye aina ya mabadiliko ambaye anaweza kubadili tabia zake kuelekea katika fikra zake katika kutekeleza majukumu yake katika jamii.

Dhana ya kujitambua (tawjih), kwa mujibu wa Bennabi ni hamasa katika harakati za ustaarabu, umoja katika malengo, na kuepukana na migogoro kati ya juhudi zitokanazo na chanzo kimoja na kuwa na malengo tofauti. Bennabi anaona utamaduni kama sifa ya mwanzo inayomsukuma mwanadamu kama sehemu ya jamii na jamii kama chombo cha mjumuiko. Mfumo wa utamaduni unaonesha muelekeo wa ustaarabu na mwisho wake katika historia.

Katika mlinganyo wa Bennabi, dini ni kiungo muhimu na kuelekeza vigezo vitatu kuelekea mchakato ya ustaarabu. Mifumo yote ya ustaarabu katika historia imemea kutokana na fikra za kidini. Hata hivyo, katika mtazamo wa Bennabi, dini haiwezi kuanzisha kazi zake za ustaarabu

kama chachu labda tu iegamie katika mchakato wa ustaarabu ambao unajumuisha, mwanadamu, ardhi na wakati katika mradi mmoja. Bennabi anafafanua kwamba ustaarabu wa kisasa umeunda mjumuiko halisi wenye kubadilika wa mwanadamu, ardhi, na wakati katika misingi ya fikra za kidini.

Bennabi anafafanua asili na chanzo cha utawala katika jamii, ambapo viungo vya kila kitendo vimo katika mambo matatu: Vitu, watu, na fikra. Kutumia njia hii ya mjumuiko katika vitu hivi vitatu unaonesha kuwa vitendo vyote, shughuli zote, na amali zote ni jumla ya watu, kuongeza jumla ya vitu, kuongeza na jumla ya fikra nyuma ya vitendo hivyo. Kufanikiwa kwa ustaarabu kunatokana na jumla ya shughuli inayotokana na jumla ya shughuli zote zinazofanywa na mwanadamu.

Katika utawala wa mtu, ustaarabu unaanzia mchakato wake na mtu mmoja aliyebadilika na kujihusisha na shughuli za kijamii. "Utawala wa mtu" wa Bennabi unajumuisha jumla ya mahusiano, jengefu au kwa ujumla wake, katika kikundi fulani, na kusisitiza umuhimu wa mahusiano hayo. Matokeo yake, hatma ya jamii katika mchakato wa ustaarabu unaegemea katika kulingana na hali halisi au ubora wa mahusiano, katika mfumo huo ulioundwa na utawala wa mwanadamu.

Kwa mujibu wa Bennabi, utawala wa fikra unajumuisha mawazo yaliyopendekezwa yaliyotokana na vyanzo vitukufu au vyanzo vingine na kufanya kazi kama mfumo ulianza na kuongoza jamii kwenye misingi ya kimaadaili. Katika ustaarabu wa Kiislamu, mawazo yaliyopendekezwa yanatokana na Qur'an na Sunna. Bennabi anazingatia ustaarabu kama matokeo ya maisha, fikra zenye kubadilika zinazohamasisha jamii iliyostaarabika toka awali kuingia katika historia kuunda fikra kwa mujibu wa mifano yake halisi.

Utawala wa fikra unatoa mtazamo na mifumo halisi katika jamii kuunda ustaarabu wake, na kuunda misingi ya awali ya binadamu wote katika jamii inaweza kufuata, utamaduni maalum. Utawala wa fikra ni muhimu katika jamii katika majukumu ya kujenga katika historia. Utawala wa vitu kwa upande wake unatoa vifaa, njia za mawasiliano, rasilimali asilia, na vitu mbalimbali vinavyohitajika katika mchakato wa ustaarabu. Utawala wa vitu unatoa mahitaji ya vitu katika harakati za kihistoria katika jamii na kuelezea nafasi ya jamii katika mchakato wa ustaarabu.

Bennabi anasisitiza kuwa hakuna shughuli ya kihistoria inaweza kutokea tawala hizi bila "mtandao wa mahusiano wa kijamii", dhana inayounganishwa na ufahamu wake katika hali halisi na mabadiliko katika jamii kutokana na mitazamo ya jamii na kiutamaduni. Mnyumbuliko wa mahusiano katika tawala tatu unaonesha na kutumia mitandao wa mahusiano ya kijamii. Mfumo huu wa utawala unatoa mahusiano ya kiwango cha chini katika tawala zote tatu kwa kitendo chochote cha kihistoria kinachotaka kutengeneza ustaarabu. Tawala hizo tatu haziwezi kufanya kazi sawasawa bila mitandao ya mahusiano ya jamii.

Kwa kuwa Bennabi alimulika katika namna ya kujenga upya jamii ya Kiislamu, kurudisha utamaduni wake, na kutenganisha na sifa hasi zilizotokana na zana za anguko, amesisitiza kuwepo kwa "Uhuru wa kisosholojia." Alama ya kuanzia katika sosholojia ni kutafsiri tena dhana ya 'jamii'. Bennabi anasema wakati jamii asilia si jamii yenye kubadilika, jamii ya kihistoria ni yenye mabadiliko. Anaongeza kuwa sifa nyingine zinafanana katika aina zote za jamii za kihistoria. Mitandao ya mahusiano ya kijamii inaunganisha wanajamii na kuelekeza shughuli za kufanya kutimiza kazi zinazofanana ambayo ni malengo maalum na mafunzo ya jamii.

# SURA YA TATU

## *Tafsiri ya Harakati za Ustaarabu*

Bennabi anautazama mzunguko wa ustaarabu kama "mfululizo wa tarakimu unaofuata mpangilio maalum katika vitu sawa lakini visivyofanana", na kupendekeza kuwa ustaarabu wa namna hii ya mzunguko (duara) na inafuata mfumo uliopangiliwa. Kila kikundi cha jamii kinakuwa na sifa za kipekee na kikundi kingine kukusu ustaarabu na kwamba kila aina ya ustaarabu ina sifa iyoipwekesha. Kimsingi ustaarabu unatofautiana katika hali zake za saikolojia ya muda (psycho-temporal) lakini zinafanana katika mfumo wa kihistoria katika ujumla wake.



Bennabi anaeleza kuwa ustaarabu unaanza na mzunguko wake wakati misingi yake mikuu inapojumuishwa katika mfumo wa fikra za kidini, na kuishia pale misingi hiyo mikuu inapokosa sifa ya mabadiliko na muingiliano. Ustaarabu wa aina yoyote unafanya kazi yake ya kihistoria mpaka ushindwe na kuacha kutimiza wajibu wake kuendeleza na kuongoza utu. Mchakato huu wa mpito wa ustaarabu unahalalisha hali ya mzunguko katika historia.

Bennabi pia anasema jamii yoyote katika mchakato wa ustaarabu utafuata mfumo unaoeleweka kuelekea katika mabadiliko. Baada ya kumaliza kipindi cha kabla ya ustaarabu, jamii itapitia hatua ya pili inayopitia hatua tatu: nafsi, sababu na uwezo binafsi.

Dhana ya mzunguko unaweza kusuluhisha matatizo kwa kutazama

nafasi mzunguko wa kihistoria na kufahamu sababu za kushindwa na mambo muhimu katika maendeleo. Dhana ya mzunguko inaweza kueleza harakati za ustaarabu na mfumo unaotawala kutathmini na kuuelewa uwepo wa masuala ya kijamii ya binadamu. Bennabi, aliyeendeleza fikra kutoka kwa Ibn Khaldun anapendekeza kuwa ustaarabu wa binadamu unaanzia katika mahali Fulani na kufuata utaratibu uliopangwa. Katika hatu ya mwisho, vigezo vya ustaarabu unapitia na kwenda katika mahali pengine. Mapitio haya yanajumuisha uwepo wa mzunguko.

Bennabi anaamini kuwa hatua tatu za mzunguko hazitokani na kuhama kibahati nasibu kutoka hali moja kwenda nyingine, badala yake muhamo huo unadhihirisha mabadiliko mengi ya ndani na uboreshwaji wa kina kwa watu na jamii. Hivyo ni lazima kuwa na mazingira maalum ya kutengeneza mseto wa kihistoria unaojumuisha vijenzi vyake vyote vitatu, ambavyo ni; watu, ardhi na wakati. Mseto huu wa mjumuiko ndio unaoasisi jamii kwa vile unavyoafikiana katika kuanzisha mwendo wake wenyewe wa kihistoria. Mpaka hapa, kanuni na maadili ya jamii vinakuwa bado hazijakamilika.



Hatua ya awali ya kila ustaarabu, fikra za kidini zinapanda mbegu kuanzisha harakati za ustaarabu. Kisha, hatua ya kiroho inaanza kumiliki maisha ya mtu mmoja mmoja na jamii. Katika hatua hii, mwanadamu aliyesambaratika atabadilika kuwa mwanadamu mwenye ushirikiano na wenzake, wakati mitandao ya mahusiano ya kijamii ni yenye nguvu. Mchakato huu unaunganisha ufahamu katika kazi za kiuhusiano kufuata sifa za fikra za kidini. Mtu mmoja anaishi katika hali hii mpya kwa kuzingatia sheria za kiroho.

Mtandao wa mahusiano ya jamii unafikia mahali pazuri wakati fikra za kidini zinazidi kupanuka. Wakati huohuo, ustaarabu sasa unaweza kuendana na matatizo na mahitaji, kuanzisha utaratibu mpya na viwango vipya. Kisha hatua ya kiroho inapungua kutegemeana na maendeleo ya jamii, kuongeza kwa matatizo yanayonasibiana na mali, na kupanuka kwa ustaarabu na kuupeleka ustaarabu katika hatua ya pili. Sababu hizo sasa zinatawala shughuli zote wakati ustaarabu ukiendelea kupiga hatua katika maendeleo. Wakati ustaarabu ukihamia hatua ya kimantiki, jamii inafurahia maendeleo mazuri ya mahusiano ya kimtandao lakini ikiwa na changamoto kadhaa. Katika muktadha wa kisaikolojia, mtu mmoja hawezi kuwa na udhibiti katika nguvu muhimu wakati wa

kutekeleza majukumu ya kijamii. Sehemu za misukumo na nguvu ya jamii zimeangukia katika kushindwa na zingine kuanguka kabisa.

Kupitia kipindi chote cha historia ya ustaarabu, mchakato wa mageuzi kutoka hatua hadi hatua inaegemea katika saikolojia ya mtu mmoja mmoja na muundo wa maadili wa kijamii ambao unakoma kurekebisha tabia ya mtu. Wakati nguvu zinazingatia mantiki zinapoanza kupoteza uwezo wake katika shughuli za mtu binafsi, ustaarabu unakabiliana na mazingira mapya wakati msukumo wa ufahamu unapotawala misukumo mingine ya kiroho na kimantiki. Ustaarabu unaingia katika hatua ya baada ya ustaarabu na vigezo vyake moja kwa moja vinaingia mjumuisho wa mtu, ardhi, na wakati. Katika hatu hii ya tatu, mtandao wa kijamii unapotea na fikra za kibinadamu au jamii hupoteza ufahamu ya kibinafsi. Katika hali hii, vurugu na kutotii sheria huchukua nafasi. Ufahamu mbalimbali unakombolewa taratibu kadri udhibiti wa roho unapopungua taratibu.

Wakati ufahamu unapokombolewa wote, hatma ya mwanadamu inaangukia katika ushawishi, hatua ya nne ya ustaarabu inaanzia hapo, pamoja na fikra za kidini zinapofikia kufanya kazi zake za kijamii. Matokeo yake ni kwamba, jamii inatawanyika na kufanya mwisho wa mzunguko wa ustaarabu. Wakati matarajio ya roho (nafsi) yanapogonga mwamba, ufahamu pia unashindwa kufanya kazi.

Bennabi anaamini kwamba ustaarabu unahusisha mizunguko yenye kuhusiana inayoanza na fikra za kidini na kumaliza pale ambapo nguvu za ufahamu za binadamu zinapotawala nguvu za kiroho na kihoja. Pia anaamini kuwa, mzunguko huu uliokamilika wa ustaarabu wenye hatua tatu unaonesha nguvu muhimu za ustaarabu na namna gani unabadilika kutoka hatua moja kwenda nyingine. Kwa kutambua kila hatua mabadiliko ya ustaarabu na kuelewa sifa zake inatusaidia kuleta mfumo wa jumla wa maendeleo na mabadiliko hayo.

Kwa kutumia mgawanyo wa jamii alioufanya Bennabi, jamii ya binadamu haiwezi kujipachika yenyewe katika mahali fulani katika maisha yake, bali, huhama kutoka katika hali moja kwenda nyingine kwa kutumia sifa za sosholojia za kijamii za maendeleo yake. Kwa hiyo, kutambua nafasi ya jamii katika muhimili wa kimaendeleo ni muhimu kubainisha hatua ya jamii husika, matatizo yanayooihusu, pamoja na utendaji wake.

Kwa upande wa muhimili unaowakilisha hatua za maendeleo, jamii ya kihistoria inachukua eneo mahususi, anasema Bennabi. Historia inaonesha kuwepo kwa hatua tatu; jamii kabla ya ustaarabu, jamii iliyostaarabika, na jamii baada ya ustaarabu. Wakati wote kila jamii inakuwa katika mojawapo ya hatua hizi na sifa zake ainishi. Bennabi anaangazia katika historia, sosholojia na saikolojia katika mbinu za kuelewa mambo yahusuyo ustaarabu. Anatumia tafsiri ya saikolojia ya jamii kuelezea safari ya kihistoria ya jamii katika kugundua sifa za sasa za ulimwengu wa Kiislamu.

Bennabi anaona kuwa mtu mmoja mmoja katika jamii kabla ya ustaarabu, kuwa ni mtu huru ambaye yuko tayari, kama Bedui wa Kiarabu katika zama za Mtume Muhammad (S.A.W.), kuingia katika mfumo wa ustaarabu. Jamii kabla ya kipindi cha ustaarabu inahitaji msukumo katika kuhamasisha ufahamu wa vitivo vya ustaarabu. Ingawa jamii ina sifa za msingi za ustaarabu yaani; watu, ardhi, na wakati, sifa hizi haziwezi kujongea bila msukumo wa fikra za kidini. Bila muingiliano kati ya watu, ardhi na wakati katika mfumo wa fikra za kidini, jamii haitaweza kufanya mchakato wake wa ustaarabu au kujionea mabadiliko ya saikolojia ya kijamii.

Maendeleo ya saikolojia ya mtu mmoja moja na jamii yataruhusu harakati za ustaarabu kwakuwa uwezo wa jamii ulilenga katika mradi wa kijamii. Wakati jamii iliyostaarabika inapoanza kujibadilisha kufikia malengo yake, ustaarabu wake hujidhihirisha. Hatua iliyostaarabika inaakisi uwezo wa jamii kupanga na kuunda mtazamo wake wa kiulimwengu na kitamaduni, Kipindi mwanadamu anapotaka kuanzisha mchakato wa ustaarabu, mtandao wa mahusiano wa jamii huimarika zaidi. Katika muktadha kama huu, jamii inaweza kulinda ustaarabu wake na kupiga hatua katika maendeleo yake. Watu wote, mmoja mmoja katika hatua hii hufurahia ulinzi wa jamii, na jamii inapofanikisha majukumu yake ya kustaarabisha.

Jamii inapofikia hatua ya baada ya ustaarabu, hapa inakuwa si yenye kubadilika tena na kupoteza uwezo wake wa kustaarabisha, na hivyo kufikia katika anguko. Hatimaye, fikra za kidini zinakoma kujumuisha vigezo vya kistaarabu, pamoja na kusinyaa kwa mtandao wa mahusiano ya kijamii. Hata hivyo bado anguko halijafika tamati. Kitendo kingine cha ustaarabu kinaweza kuilinda jamii kutokana na hatima na mabadiliko ya njia yake ya anguko. Pindi jamii inapokosa muundo

wake wa kitamaduni, utawala wake wa kifikra unaingia katika kipindi cha vurugu na hapo utamaduni wake unakosa dhima ya kustaarabisha. Bennabi amegundua mkanganyiko kuhusu hatua na kutoeleweka kwa sifa zake miongoni mwa wasomi. Mkanganyiko huu wa hatua utafanya juhudi yoyote ya kutatua matatizo ya jamii kuwa ngumu.

Bennabi anajaribu kutatua tatizo la hali ya sasa katika ulimwengu wa Kiislamu kwa kumulika katika hatua yake ya tatu, ambapo jamii imepoteza fikra zake za awali au tabia ikilinganishwa na hatua zingine. Kutatua matatizo yake, jamii lazima irejee katika asili yake na tabia ya kubadilika kwa kumtengeneza mwanadamu mpya aliyekombolewa katika sifa za hatua ya tatu ya ustaarabu yaani hatua baada ya ustaarabu wa mwanadamu. Baada ya hapo, anaweza sasa kuingia katika mzunguko mpya wa mjumuisho pamoja na ardhi na wakati kwa kushirikisha fikra za kidini. Beannabi anaona umuhimu wa kufahamu masuala ya kihistoria na sababu za kuanguka kimaendeleo. Matatizo ya kijamii ni ya kihistoria: kile kinachofaa kwa jamii katika hatua fulani ya maendeleo inaweza kuwa na madhara katika hatua nyingine.



Pia Bennabi anachanganua mabadiliko ya jamii kutoka katika mtazamo wa kisaikolojia ya jamii na kuingiza dhana tatu za zama za maendeleo ya kisakolojia ya jamii. Hapa anaonesha dhana nzima ya mahusiano mnyumbuliko kati ya utawala wa watu, vitu na fikra zinazotoa maana ya dhana ya zama tatu. Bennabi anasema jamii yoyote ina mfumo wake wa utamaduni mtambuka ambapo utawala wa vitu, watu, na fikra vinafanywa viingiliane na vitendo vya jamii vinavyofanyika kwa pamoja.

Jamii katika zama zake za mwanzo inaunda hukumu na maamuzi yake kulingana na vigezo vinavyowekwa na utawala wa vitu. Asili na ubora wa hukumu hizo zinaendana na mahitaji ya binadamu ya kijima na kumfanya awekwe katika utawala wa vitu. Bennabi anaendelea kufafanua kuwa jamii ya kibinadamu imepitia zama za vitu katika hatua kabla na baada ya ustaarabu. Jamii ya sasa ya Kiislamu, inaathiri viwango vya kisaikolojia na vya kiroho (maadili), kijamii, kitaaluma, na viwango vya kisiasa, wakati utamaduni unapoelemea katika vitu, vitu vinakuwa ndio kipaumbele katika vigezo, hukumu zitakuwa idadi kuliko ubora, na hapo kila kitu kitahukumiwa kwa vipimo vya vitu, na si vigezo (thamani).

Katika zama zake za pili, jamii inaunda hukumu zake kulingana na viwango vya kisasa vya kibinadamu au kwa mfano, kuchukua kutoka katika utawala wa watu, na si vitu. Katika hatua hii utawala wa vitu na fikra unapaswa kutumika pamoja na utawala wa watu. Hapa Bennabi anapigia mfano wa Jahil, yaani, jamii kabla ya Uislamu wa matumizi ya utawala wa watu ambao ulifungamanishwa na mipaka ya kikabila. Katika jamii ya sasa ya Kiislamu, kuna makutano kati ya kujikita katika vitu na watu, ambao kimsingi Bennabi anasema ni wenye madhara hususan katika vigezo vya kiroho (maadili) na vya kisiasa.

Mwandishi anaamini kuwa dhana ya zama tatu ni zana muhimu katika kupima harakati za jamii katika kipindi cha historia, na kupima sifa zinazoongoza za jamii katika muda maalumu kutambuakama jamii inastawi au inaanguka. Kitendo cha jamii kinapaswa kuonwa kama shughuli inazoingiliana, pale ambapo utawala wa vitu unapochanganyika na tawala nyingine za watu na fikra. Kwa kawaida utawala mmoja ndio hutokea kutawala mingine, ukitofautiana kutoka jamii moja na nyingine katika masuala ya fikra na tabia.

Dhana ya zama tatu ungeweza kutumika kama kipimo cha ukomavu wa kisaikolojia ya jamii, uelekeo wa mchakato wa kustaarabisha, mpangilio wa shughuli zake, na kuhamisha kwa sifa kutoka hatua moja hadi nyingine katika kipindi chote cha historia. Vilevile, kutawala kwa utawala mmoja katika tawala mbili zingine unaonesha jamii ilipo katika harakati za kihistoria. Zama hizi zinawakilisha sifa za kijamii na mazingira ya kiutamaduni yanayotawala na kushawishi jamii katika hatua yoyote ya maendeleo yake.

Bennabi aliuweka Ulimwengu wa Kiislamu katika hatua ya kabla ya ustaarabu ambapo ulijitahidi kuingia katika mchakato wa kustaarabika. Alifafanua harakati za ustaarabu kupitia viwango mbalimbali vya tathmini kwa ajili ya uelewa mpana wa mchakato unaobadilika wa ustaarabu katika historia. Dhana zake za mzunguko, hatua tatu, za zama tatu, ni hatua ya juu kabisa ya za uchambuzi wa hali moja.

Maendeleo ya jamii katika mchakato wa ustaarabishaji yanahifadhiwa ki-ubora na ki-idadi, anasema Bennabi, katika mtandao wa mahusiano ya jamii, unaoonesha hatua za jamii katika kipindi cha historia. Anafafanua kuwa mchakato wowote wa kustaarabisha unaanza kabla ya kuwepo kwa tawala zake tatu. Kuwepo kwa utawala wa watu ni hatua ya

mwanzo katika uundaji wa mtandao wa mahusiano ya kijamii. Wakati huo jamii inafanya kazi wakati tawala za fikra na vitu bado vingali virahisi. Utawala wa watu hubadilika na kuingia katika mpango mpya wa uhusiano. Mtandao wa mahusiano ya kijamii yanaanza kufanya kazi wakati tawala nyinine mbili za fikra na vitu zikiwa bado changa.

Utawala wa fikra una kazi kubwa ya ulinzi wa kijamii wakati ukihusishwa kimadhubuti na mtandao wa mahusiano ya kijamii. Utawala wa fikra pekee hauwezi kuhalalisha maendeleo ya kistarehe ya ustaarabu. Badala yake, unapaswa kushirikiana na mtandao wa mahusiano wa kijamii. Historia ya jamii si lolote zaidi ya historia ya mtandao wa mahusiano ya kijamii ulioundwa mwanzo na fikra za kidini.

# SURA YA NNE

## *Kigezo cha Ndani cha Kijamii*

Kwa kutumia maana ya Ritzer ya kigezo cha ndani cha kijamii, sura hii inajikita katika matokeo ya vigezo hivi katika mtazamo wa Bennabi. Historia ya maisha ya Bennabi (biografia) imetawanyika kidogo na historia ya maisha yake aliyoandika mwenyewe (autobiografia) imeanza toka kuzaliwa kwake mwaka 1905 mpaka 1939. Kutokuwa na mali katika maisha yake yote kumeelezwa katika vitabu vyake, machapisho yake ya zama hizi na rekodi zake za kihistoria katika zama zake.

Malik Bennabi alizaliwa mwaka 1905 katika familia ya kimasikini, Mashariki mwa Aljeria. Mazingira ya Kiislamu ya jamii yake yalitengeneza muonekano wake na kuilinda jamii ya Kiislamu dhidi ya nguvu za kikoloni katika utamaduni na ustaarabu wao.

Visa alivyosimuliwa na bibi yake viliujenga wasifu wake kama mwenyewe alivyosema kuwa "Visa vya kiimani kutoka kwa bibi vilikuwa vikiujenga wasifu wangu, na kwavyo najua utukufu uko katika mafanikio yanayopatikana kwa vigezo vya Kiislamu na maadili".

Chini ya utawala wa Ufaransa, Bennabi alishuhudia uhamaji wa pamoja wa familia nyingi, wakiwemo ndugu zake, kutoka Aljeria kwenda nchi za Mashariki za Kiarabu. Kupinga huku dhidi ya utawala wa kikoloni ulifanya mabadiliko ya haraka katika sura ya kijamii na kiuchumi ya Aljeria. Mazingira ya Kiislamu ya awali yaliporomoka,

maisha yaliyokuwa mwanzo yaliparaganyika, na kuwa katika makundi kulifanywa kuwa hatari. Bennabi aligundua umuhimu wa mahusiano ya kijamii katika uwanda mdogo na katika uwanda mkubwa wa jamii.

Katika jumuiya ya Bennabi, Zawiyah, taasisi iliyokuwepo muda mrefu na ya asili, ilifanya kazi kubwa sana ya kulinda na kuhifadhi mafunzo ya Kiislamu baada ya kudorora kwa ustaarabu wa Kiislamu, kama ilivyokuwa katika elimu na fasihi rasmi ya Kiarabu. Wasimulizi wa visa walitunza utamaduni maarufu, wakati msikiti na madarasa vikifanya kazi kubwa katika elimu ya Bennabi. Alisoma lugha ya Kiarabu, fasihi, msukumo wa kijamii, utamaduni, na ustaarabu.

Katika kitabu chake cha kwanza, Bennabi alifanya tafsiri ya mada katika Qur'an na kufanya ufafanuzi wa nadharia zake katika mazingira tofautitofauti ya kijamii na kiutamaduni. Msingi wake mkuu katika utafiti katika dini uliongozwa na mchanganuo kuhusu dhima yake na jukumu lake katika mchakato wa ustaarabu. Kwake Bennabi, dini anaiona kama mfumo uliotengenezwa kulingana na ulimwengu ulivyo, kama sheria inayofanya sifa za kiroho za mwanadamu. Bennabi aligundua Uislamu katika mtazamo wake wa kiulimwengu alipokutana na wanazuoni wengi wa Kiislamu pamoja na wanaharakati nchini Ufaransa.

Tatizo la elimu katika ulimwengu wa Kiislamu lilikuwa msingi mkuu aliotaka kuumulika Bennabi. Malengo, mbinu, namna, na majukumu vilikosekana, hususan nchini mwake (Aljeria) chini ya utawala kandamizi wa Kikoloni. Mifumo miwili ya kielimu ilichagiza fikra na imani yake katika kutafuta kuporomoka kwa maadili katika mfumo wa kitamaduni na kuendelea kwa mfumo wa elimu wa Ufaransa ya kisasa (Ufaransa na nchi za Magharibi).

Wakati mfumo wa kitamaduni ulipokuwa katika hali ya kutisha, mfumo wa kuendelea kwa mfumo wa elimu ulikuwa ukistawi. Mfumo huu wa pili ulipata fursa ya kuendeleza mbinu na maelengo yake na kujihakikishia ulinzi madhubuti wa utawala wa kikoloni. Hata hivyo, malengo yake (ya kidunia) na malengo ya usasa yaliukoroga mfumo wa ustaarabu wa Uislamu, hali iliyomea katika umakini katika kipindi chote cha maisha yake na taaluma yake.

Bennabi aligundua na kurekodi mabadiliko yaliyokuwa yakitokea katika maisha na fikra katika mazingira ya Ulaya na ya Ki-Aljeria. Mazingira haya mawili yalishawishi dhana zake kwa mwanadamu wa

asili ni mwanadamu wa ustaarabu. Ameshuhudia mabadiliko mapya ya kifikra katika jamii ya kitaaluma ya Uislamu. Harakati za 'Ulama' zilisimamishwa katika jamii ya Kialjeria katika mtazamo na mbinu zihusuzo mabadiliko ya jamii.

Historia ya Bennabi kama mwananchi wa Aljeria iliyotawaliwa na mkoloni, mwanafunzi katika mifumo miwili ya kielimu, na kuwafahamu wakoloni wa Ulaya pamoja na dhana ya "kutawalika" kama chombo cha kufanyia uchanganuzi wa mambo ya kisaikolojia ya sasa ya Waislamu.

Ufahamu wa Bennabi katika fikra za Kiulaya zilimnyanyua kitaaluma na ufahamu wa kisiasa, na hivyo malengo yake kuhamia katika filosofia na sayansi ya jamii na kisha kutopea katika mwanaabadiliko wa fikra za Kiislamu, harakati za ukombozi na juhudi za kuihuisha nchi yake ya Aljeria na ulimwengu wa Kiislamu kutoka katika uhandisi aliyokuwa nayo mwanzoni. Aliona umuhimu wa harakati za'Ulama' nchini Aljeria na kuendeleza fikra za islah (mabadiliko), na umoja wa Maghrib (Afrika Magharibi). Bennabi alivutiwa na harakati za mabadiliko ya 'Ulama' katika kuhakikisha jamii ya Aljeria inakuwa huru mpaka walipokabidhi utawala wa kijamii kwa wanasiasa. Aliamini umuhimu wa shughuli za kielimu na kitamaduni katika harakati za kisiasa.



Kama mkimbizi wa kisiasa nchini Misri, Bennabi alianzisha mahusiano na wasomi na taasisi mbalimbali, kuwashawishi wasomi wa Kiarabu kujikita katika mambo yahusuyo kurudisha ustaarabu na ustawi wa Umma wa Kiislamu. Bennabi alifariki katika jiji la Algiers mwaka 1971, akiacha muongozo kutoka kwa mwanazuoni mkubwa kabisa ambaye kazi zake hazikuwahi kufananishwa na nyingine katika kipindi cha sasa.

Mahusiano ya Bennabi yalitegemea nadharia mtambuka katika vigezo vya ndani vya kijamii. Aliamini katika kufanya kazi pamoja na mahusiano madhubuti na wasomi mbalimbali wa Kiislamu na nchi zinazoendelea ili kutafuta suluhisho matatizo tanzu ya kimaendeleo. Miongoni mwa mahusiano yake imara zaidi ni yale ya harakati za mabadiliko katika ulimwengu wa Kiislamu uliowakilisha na 'Ulama'.

Unyenyekevu wa Bennabi katika Uislamu na kuvutiwa na Ibn Khaldun zilifanya uchanganuzi wa dhana ya kujiona dhaifu kwa wasomi wa Kiislamu dhidi ya utamaduni wa Kimagharibi. Anasema wasomi wa utamaduni wa awali ('Ulama') wasingeweza kufikia malengo yao kwasababu ya mfumo wa zama za al-Muwahhid. 'Ulama' walijikita

katika utukufu na uhifadhi wa mafundisho wa Kiislamu, pamoja na kudumisha, kubadilisha nafsi na mitazamo yao katika utamaduni baada ya zama za al-Muwahhid kwenda katika utamaduni mpya.

Bennabi alishawishika na wanazuoni na waandishi wa mwanzo wa Kiislamu kama akina; Ibn Taymiyyah, Ibn Khaldun, na Ibn Abd al-Wahhab na kujiona yeye mwenyewe kama zao la mkufu wa mabadiliko. Baada ya uzoefu wake katika nchi nyingine za Kiarabu alipanua uchanganuzi wake na kuongeza fikra za kidini, na kuchunguza maelezo mbalimbali wa mambo ya jamii, pamoja na kazi ya dini katika mabadiliko ya kihistoria.

# SURA YA TANO

## *Kigezo cha Nje cha Kijamii*

Kwa mujibu wa mbinu mtambuka, vigezo vya nje ya kijamii vinajikita katika uwanda mkubwa wa uchambuzi na kuelezea vipengele mahususi. Vigezo hivi vinatazama katika fikra msingi za taasisi na kihistoria. Vigezo hivi vinafanya vigezo vya nadharia mtambuka vinavyohamia katika uwanda mkubwa kutazama katika jamii kubwa zaidi na matokeo yake katika maendeleo ya kufanyika kwa nadharia. Kigezo cha nje cha kijamii kinasisitiza uhusiano kati ya mchakato wa kutengeneza nadharia na taasisi mbalimbali, miundo ya taasisi, na kazi zingine za kijamii zenye uhusiano wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja na maendeleo ya mtazamo au nadharia.



Bennabi alilenga katika kutatua matatizo yahusuyo ustaarabu wa Kiislamu katika muktadha wa kufanyika kwa ukoloni na harakati za kuondoa ukoloni kwa kutumia sosholojia kufahamu muktadha mpana wa kijamii na kihistoria. Bennabi aliamini ukoloni ulikuwa sehemu ya ajenda kamili ya ustaarabu wa Kimagharibi, na hivyo kuhitaji majibu ya kiustaarabu kutoka ndani ya mfumo huo.

Sayansi, anthropolojia, akaelojia na sosholojia za Kimagharibi zilisaidia katika kile kilichodaiwa kuwa malengo ya kistaarabu kuwastaarabisha wazawa, washenzi, waliopitwa na wakati. Maneno hayo yalitumika kuwatia udhaifu watu waliotawaliwa na waliokuwa na ustaarabu wao. Hapo ilifuata hali ya kutofautisha baina ya ustaarabu wa kikoloni na

ustaarabu wa aina nyingine kwa kuingiza na kulazimisha viwango vyao kwa jamii za kizawa. Hii iliwagawa wananchi na kuyabagua mataifa ya Kiislamu katika mitazamo ya kikabila, na lugha hivyo kuhatarisha na kubomoa umoja wa Umma.

Jamii ya Kialjeria kabla ya zama za ukoloni ilikuwa katika hatua ya baada ya kustaarabika, yaani hatua ya tatu katika falsafa ya Bennabi ya ustaarabu. Kisosholojia, jamii hiyo ilikuwa imara na maendeleo ya hali ya juu ikilinganishwa na kipindi chote cha ukoloni. Aljeria iliishi maisha mazuri, uimara katika medani ya siasa, maendeleo ya kiuchumi, maendeleo ya kitamaduni, ustawi wa kijamii, pamoja na elimu. Jukwaa lake la wasomi ('Ulama') lilieneza elimu na mafunzo ya Kiislamu na kuhifadhi utambulisho wa Mualjeria.

Kwa bahati mbaya, maendeleo na utajiri havikwisha. Harakati za kikoloni zilipitia katika hatua hatua kuu nne zinazoweka alama katika jamii ya kizazi kijacho ya Waaljeria. Hatua ya Uvamizi wa Ukoloni na Upinzani (1830-1848) ilianza na sera ya "uvamizi mdogo" wa Ufaransa. Sera hii ililenga kuwatenga Waaljeria dhidi ya vitendo vya kipinzani dhidi ya utawala wa kikoloni na kubadilisha mifumo ya Waaljeria ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kidini.



Hatua ya pili ya upinzani ilihusisha kuenzeza utawala wa kikoloni (1847-1871) ambao uliwagawa Waaljeria na kuwakandamiza Waaljeria wazawa. Hatua ya ukoloni kamili na ufahamu wa wazawa (1871-1919) uliendeleza zaidi ukandamizaji kwa Waislamu wa Kialjeria na kupanua ongezeko la walowezi. Katika hatua ya muamko wa Waaljeria, (1919-1962), ukoloni ulifikia hatua yake ya juu sana wakati ambao wanamabadiliko Waislamu wa Kiafrika na kurudi katika hali ya kawaida vilijitokeza miongoni mwa wasomi wazawa na wanasiasa.

Mwisho, nguvu kubwa ya Uislamu, ambao katika karne zote uliwapatia Waaljeria hali ya utambulisho ya ujumla, na kuhamasisha upya miaka ya 1920 na 1930. Wakati wa hatua ya nne ya ukoloni, mgogoro kati ya wazawa na utawala wa kikoloni ulifikia hatua mbaya sana.

Kwa mtazamo wa Bennabi, Aljeria imekuwa katika hali ya vurugu kwa karne tatu, ikilinganishwa na historia tukufu na viwango vya ustaarabu wa Kiislamu. Vurugu hizo katika nyanja za ndani na nje zinawezesha mnyumbuliko wa kutawala (kikoloni) na ukoloni wenyewe. Kwa Bennabi, ukoloni umechangia uwepo wa vurugu katika muonekano

wake wa moja kwa moja katika nyanja zote za maisha. Kufikia malengo ya kikoloni, hususan katika ulimwengu wa Kiislamu, ukoloni ulilenga kukandamiza mchakato wowote wa ustaarabu kwa kuanzisha mazingira ya bandia kati ya viungo vya jamii.

Kujibu hayo, vuguvugu la ukombozi wa Kialjeria ulianzishwa chini ya juhudi kubwa za 'Ulama' katika kiwango cha kitaaluma na kidini na pia chini ya wanasiasa katika kiwango cha siasa, na hivyo kuonesha uhusiano kati ya nadharia ya Bennabi na nadharia ndogo mbili za kuuondosha ukoloni, yaani ya kimageuzi na ya kisasa.

Bennadi anaona kuwa kuondosha tatizo la ukoloni na sababu za kutawaliwa (kikoloni), tunapaswa kutatua mambo ya msingi katika kitovu cha mgogoro wote kwa kuanzia na mfumo mchanganyiko. Nadharia ya kistaarabu ya Bennabi inaweza kuchambua mazingira ya binadamu na mabadiliko ya kijamii ndani a mfumo wa ustaarabu kama mfumo linganifu.

# SURA YA SITA

## *Kigezo cha Ndani cha Kitaaluma*



Utafiti huu unajadili vigezo vya ndani vya kitaaluma zinazounda kigezo cha tatu kwa kutumia nadharia mtambuka katika aina yake ndogo. Inahusiana na stadi ya sifa za kiutambuzi katika uga wa ustaarabu na iko ndani ya eneo la stadi ya Bennabi katika kuondosha matatizo katika ulimwengu wa Kiislamu. Inatambua nadharia kuu ya utambuzi, mitazamo, kubadilika kwa nadharia, na zana za nadharia mtambuka kwa ujumla kuchanganua nadharia zilizopo na kuanzisha zingine.

Nadharia kuu mbili zimetawala katika stadi ya ustaarabu yaani: filosofia ya historia na sayansi ya jamii. Bennabi anaona stadi ya ustaarabu kama tasnia ya kipekee ambayo mbinu yake na dhana zake zinatokana na sayansi ya jamii. Kwa kutumia ufahamu wake wa Qur'an na masomo ya dini ameweza kuzuia dhana zinazoegamia katika vitu na za kidunia zihusuzo ufahamu na mabadiliko ya kihistoria. Kwa kutumia vigezo vya ndani vya kitaaluma vya nadharia mtambuka katika stadi hii kugundua ufahamu wa Bennabi katika nadharia zinazotawala kwenye ustaarabu.

Sura hii inatumia uchanganuzi wa maudhui kupata vyanzo vya baadhi ya fikra za wasomi wa awali. Uchambuzi wa nadharia zinazotawala na mitazamo tofauti tofauti unaunganisha kati ya dhana, istilahi na mbinu pamoja na asili zake katika tasnia husika na mitazamo iliyotawala wakati wa maisha ya Bennabi kupitia kipindi chote cha historia.

Ndani ya nadharia ya falsafa ya historia, mitazamo mitatu inatumika katika stadi ya ustaarabu na nadharia zinazohusiana nazo yaani; mtazamo wa mzunguko (mduara), mtazamo wa maendeleo, na ule wa bega-kwa-bega wa wanadamu katika tofauti zao. Mitazamo hii inaunda mitazamo ya mabadiliko ya kihistoria katika hali za kibinadamu na mitazamo mikuu ambayo imegusia jambo la ustaarabu kwa kutaja na kufafanua mifumo katika mabadiliko ya kihistoria.

Karne ya 19 ilikuwa ya mchakato wa kihistoria, ikiongozwa na akina Hegel, Comte, na Marx, ilishuhudia historia kama endelevu na kuchangia katika kazi ya Bennabi juu ya ustaarabu. Katika mbinu mnyumbuliko ya Hegel, historia ni kisa cha maendeleo ya ustaarabu na uhuru wa mwanadamu. Marx, nguli mwingine katika karne ya 19, alipendezwa na fikra za Hegel. Wakati Hegel akitumia fikra za mnyumbuliko, Marx anatumia mnyumbuliko wa kiuchumi. Akishajiishwa na maendeleo, Comte anatumia nadharia ya Darwin ya mabadiliko na maendeleo ya sayansi ya vitu katika hali za mwanadamu na mabadiliko ya kihistoria. Mchanganuo mkubwa wa nadharia katika nyanja ya utafiti wake ni ufafanuzi wake wa harakati za kihistoria, hatua na sababu zake.

Bennabi anasema wanahistoria karibu wote wamejaribu kukusanya matukio ya kihistoria badala ya kutengeneza mfumo wa kufanya uchanganuzi wa matukio hayo. Yeye aliona uhusiano kati ya fikra za mkanganyiko au mnyumbuliko ya Hegel na ile ya Marx kwamba sababu mkanganyiko zinazo changia mabadiliko ya kijamii ni za kiuchumi. Bennabi anakubaliana na fikra za Hegel kama chachu ya mabadiliko. Hata hivyo, anaona nadharia ya Marx ya mahitaji ya mwanadamu haiwezi kueleza mnyumbuliko wa kuzaliwa kwa ustaarabu.

Bennabi anakosoa mtazamo wa maendeleo wa kihistoria kwa kuwa kinadharia zaidi kuliko kihistoria na pia kutokana na misingi yake ya kuegemea katika fikra za kiulaya. Mtazamo huu umeangazia katika vigezo vya mabadiliko ya kihistoria na kutupilia mbali upana wa ustaarabu kama hali yenye sura nyingi. Bennabi alishawishika zaidi na mtazamo wa kimzunguko (cyclical), ambao Ibn Khaldun na Toynbee ni wasomi wanaoongoza katika mtazamo huo. Bennabi anajiona kama mrithi wa mtazamo huu ambao, unatofautisha mifumo katika mabadiliko ya kihistoria na kufafanua mifumo hii kama mzunguko. Wasomi wamefikia katika mifumo ya kiulimwengu ya mabadiliko ya kihistoria baada ya kutathmini taarifa za wanahistoria.

Katika Muqadimah, Ibn Khaldun alikuwa muasisi wa uchunguzi wa historia kutambua sheria na mifumo yake. Utafiti wake katika asili ya jamii na mabadiliko ya kijamii ilimfanya aanzishe kilichoitwa 'Ilm al-Umran, sayansi ya ustaarabu, ambayo kwayo maendeleo na mchakato unachangia mwelekeo wa ustaarabu. Dhana yake ya 'Asabiyyah, ni nguvu inayohamasisha mabadiliko ya kihistoria katika kustawi, kukua na kutawanyika kwa tawala na nchi nyingi.

Toynbee anaona historia ya dunia kama muendelezo wa ustaarabu na kuuona ustaarabu kama matokeo ya changamoto mnyumbuliko na majibu na pia kama hatua za kukua na kuanguka. Anasisitiza, asili ya ustaarabu kama kitengo cha kiujumla au kilicho chepesi kufahamika cha mabadiliko ya kihistoria. Kama Ibn Khaldun, Toynbee anafafanua mchakato wa kustaarabisha ambao lazima uishie katika kuvunjika na kuanguka kwa ustaarabu.

Wasomi wengi wanakubaliana kuwa Bennabi ni Ibn Khaldun wa pili kwa fikra zake, mbinu zake na mazingatio yake. Dhana zote za mwanzo katika historia na mzunguko wa ustaarabu umevutia umakini wa Bennabi. Aliamini dhana ya vuguvugu la kimzunguko ambalo linaruhusu mjadala wa hali za maendeleo endelevu na sababu za kuanguka. Bennabi amepanua mtazamo wa Ibn Khaldun kama kitengo kinachofahamika vizuri cha utafiti wa kihistoria jamii kutumia ustaarabu kama kitengo cha utafiti wa kihistoria. Matumizi ya ustaarabu kama kitengo cha uchanganuzi wa kihistoria, dhana yake ya mzunguko na kuunda kwa changamoto na majibu pia umeshawishi mtazamo wa Bennabi.

Bennabi ametumia mbinu ya sayansi jamii kuchanganua na kutathmini matukio ya wakati wake na kujadili majukumu ya dini katika mchakato wa ustaarabu. Kwa mtazamo wake wa sosholojia na saikolojia zilikuwa muhimu sana kuusukuma ustawi wa Kiislamu. Aliona dini kama chombo cha kujumuisha sifa za kijamii na chachu ya ustaarabu kuingia katika mahusiano mnyumbuliko. Bennabi anamtazama binadamu kama chombo cha mwanzo cha ustaarabu kinachoanzisha mabadiliko. Hakuridhishwa na nadharia mbili zinazotawala za falsafa ya historia ya sayansi ya jamii, mitazamo mitatu, na mitazamo mbalimbali katika uga wa ustaarabu.

# SURA YA SABA

## *Kigezo cha Nje cha Kitaaluma*

Kigezo cha nne katika mtazamo wa nadharia mtambuka kinajumuisha sababu (vigezo) za nje za kitaaluma kama mbadala wa nyanja nyingine za kitaaluma kwa ajili ya kupata fikra, zana, dhana, na nadharia katika uchambuzi wa nadharia. Kigezo hiki cha nje cha kitaaluma kinajikita kwenye ushawishi wa sayansi za jamii na tasnia zingine za utafiti za hapo mwanzo ambazo zinafahamika kwa kukifanya kuwa cha nje katika ustaarabu. Katika mtazamo wa Bennabi, kigezo hiki cha nje cha kitaaluma kinajumuisha matokeo ya Qur'an na Sunna, fikra ya kimamadiliko ya kidini katika ulimwengu wa Kiislamu, saikolojia, sayansi asilia, filosofia, na shughuli mbalimbali za kitaaluma ambazo ni za nje katika utafiti kuhusu ustaarabu na nadharia zake kuu mbili za awali.

Bennabi alitengeneza tafsiri ya Qur'an akizingatia maendeleo ya kisasa ya kisayansi na maendeleo katika sayansi za jamii. Katika kufafanua dhana ya mzunguko ya mabadiliko ya kihistoria Bennabi anatumia Qur'an kuelezea kazi ya fikra ya kidini katika mchakato wa ustaarabishaji wa Qur'an katika historia. Bennabi anachunguza ni kwa vipi dini inafanya katika mageuzi maisha ya mwanadamu katika mchakato wa ustaarabu.

Moto anaoutumia Bennabi katika mtazamo wake unatumia aya ya Qur'an, "Hakika, Allah hatabadilisha hali za watu mpaka watakapobadilisha nafsi zao wenyewe". Moto huu unaelekeza uchambuzi wa hadhi ya

mwanadamu na kutawala kwa vigezo vya kibinadamu katika mabadiliko ya kihistoria na katika mabadiliko katika hali za wanadamu. Bennabi anasisitiza kwamba kuanzisha mchakato wa kustaarabisha, jamii lazima ibadilishe hadhi ya mwanadamu kutoka katika asili yake na kufuata taratibu zilizomuelekeza namna ya kuishi.

Kanuni za Qur'an zinatusaidia kufahamu mabadiliko ya kihistoria na jukumu la dini katika mchakato, wakati uchunguzi wa kihistoria unasaidia kuthibitisha kanuni za Qur'an na kutoa uthibitisho thabiti. Bennabi anapingana na fikra ya usasa au ya kidunia ambazo kimsingi zinakataa kuwa dini haihusiki katika jukumu lolote katika ustaarabu wa mwanadamu. Anajitahidi kuthibitisha kwamba Qur'an na Muongozo kutoka kwa Allah kama inavyotajwa katika mafundisho ya mitume wote kama ni kitovu cha ustaarabu wa mwanadamu.

Kutatua tatizo hili la kurudi nyuma kwa ulimwengu wa Kiislamu, tunapaswa kuzingatia mifumo ya kudumu ya historia iliyotajwa katika Qur'an na kufafanuliwa na Ibn Khaldun katika dhana zake za kimzunguko za mabadiliko ya kihistoria, mifumo ya kiulimwengu, na sheria katika historia. Qur'an na Sunna, katika muktadha wa nadharia mtambuka, ni vigezo vikuu vya nje vya kitaaluma vilivyoshawishi mtazamo wa Bennabi wa ustaarabu.



Fikra za kimageuzi katika ulimwengu wa Kiislamu zinatumia fikra za islah, tajdid, na nahdaj, vitambulisho vya harakati (mageuzi, kurudisha katika hali yake ya mwanzo, na ustawi). Haya yote ni ufafanuzi wa nadharia kuu zilizojitokeza katikati ya karne ya 18. Harakati za Ibn Abd al-Wahhab zililenga kuuhuisha wa mtazamo msingi wa kiujumla wa Uislamu, ambapo wazo la upekee unaweka msingi wa kanuni zote za mnyumbuliko. Al-Afghani, mwanazuoni mwingine wa fikra za kimageuzi katika ulimwengu wa Kiislamu anakubaliana na nadharia kuu hii ya mageuzi kwa kusema kwamba mafundisho ya asilia ya Uislamu ni muhimu katika kutokea kwa mageuzi ili kufanikiwa. Bennabi ametumia fikra za msingi za harakati hizo katika nyanja zake za kitaaluma.

Wanamageuzi nchini Aljeria hawakufanyia kazi kurudi nyuma kutoka katika mtazamo wake mpana. Bennabi anageukia saikolojia kwa ajili ya mtazamo wenye mpangilio mzuri, kwa nia ya kufahamu kwa vipi maisha ya binadamu yanaweza kubadilishwa na kuendelezwa kulingana na kupata malengo ya mchakato wa ustaarabu. Anahitaji kufahamu kwa

vipi fikra za kidini zinaingia katika mjumuisho wa sifa za kijamii na kunyanyua malengo ya mwanadamu.

Bennabi anawatumia Freud na Jung kuzingatia nafasi na majukumu ya dini, kwa kushirikisha saikolojia ya kimmaendeleo ya Piaget. Bennabi anasema fikra za kidini zinatoa uhuru kwa nafsi za wanadamu kutoka katika sheria za maumbile na kusaidia na sheria za kiroho. Dini inaiongoza tabia ya mtu mmoja mmoja kuelekea katika nguvu muhimu na kuiwezesha jamii kutekeleza shughuli za pamoja. Freud amemsaidia Bennabi kufahamu majukumu ya muda ya kisaikolojia ya dini katika kubadilisha sehemu yake ya ndani ya maisha ya mwanadamu na kuongoza nguvu muhimu za mtu mmoja mmoja na makundi kuelekea majukumu yenye mafanikio katika mchakato ya ustaarabishaji.

Wakati fikra za kidini zikiongoza mchakato wa kustaarabisha unapoteza majukumu yake ya mnyumbuliko, mchakato wa ustaarabishaji unadorora na kushindwa kufanya kazi kwa pamoja na fikra zake au mifano yake kuntu. Ingawa Bennabi amechukua dhana ya hatua kutoka kwa Ibn Khaldun, anatumia saikolojia ya maendeleo ya kisasa kuchambua maendeleo ya jamii ya kisaikolojia na kijamii. Akishawishiwa na Piaget, Bennabi anasisitiza kwamba mtu mmoja mmoja na jamii zinaonekana kupitia hatua tatu za kihistoria, yaani; umri wa kitu, umri wa mtu na umri wa fikra.

Falsafa ni kigezo cha nne cha kitaaluma kumshawishi Bennabi katika mtazamo wake wa ustaarabu. Falsafa, fikra za KiCartesia na mjadala wa kisasa vilikuwa vyanzo vya nje, pamoja na fikra za Ibn Tufayl, Daniel Defoe, Ibn Rushd, and al-Ghazali. Moja ya mchango muhimu kabisa kutoka kwa Descartes ni mbinu ya uchambuzi. Ametumia njia mbili za uchambuzi, ambazo kimsingi zinahusiana na vigezo vya kimuundo wa ustaarabu na kazi za vigezo hivyo katika mchakato wa ustaarabishaji.

Bennabi ni mmoja kati ya wananadharia wachache walioukabili ustaarabu katika hali ya nyanja nyingi. Mchango wake unaweza kuchukuliwa kama maendeleo muhimu na mbadala katika nadharia kuu za asilia zilizotawanyika na kupingana. Bennabi ni muhimu kama mjenzi wa mfumo na mwananadharia wa mtazamo mtambuka.

Vigezo vya nje vya kijamii vilimsaidia kutambua wapi anaanzia katika kutafiti ustaarabu. Msisitizo wake katika mazingira ya Aljeria na katika ulimwengu wa Kiislamu wakati wa kipindi chake umemuwezesha kuunda mtazamo wake kwa suluhisho la kutosha katika matatizo mbalimbali yayoikabili jamii na umma. Kwa upande wa mbinu, Bennabi alitumia mbinu za wanahistoria, wakati kwa upande wa kitaaluma na kiutambuzi, ametumia mbinu kutoka katika tasnia mbalimbali katika kutafuta ufumbuzi wa masuala ya ustaarabu kwa kutumia vigezo vyake vikuu vitatu, yaani; kihistoria, kijamii, na kitamaduni.

Vigezo vya nje vya kitaaluma vinajumuisha Qur'an na Sunna, fikra za kimageuzi za kidini katika ulimwengu wa Kiislamu, saikolojia, sayansi asilia, falsafa, na shughuli nyingine za kitaaluma ambazo ziko nje ya tasnia husika ya utafiti na mitazamo yake ya asili inayotawala.

Kunapaswa kuwa na msisitizo zaidi katika mtazamo wa kutumia stadi za mambo tofauti tofauti za ustaarabu ambao Bennabi ameuunda na kuuendeleza, na katika kuchukua mbinu mtambuka katika kutafiti uundwaji na uendelezaji wa fikra, mbinu, nadharia, na tasnia za utafiti kwa ajili ya umuhimu wake katika kupata ufahamu mpana juu ya mwanzo na kukua kwa ufahamu.

## KUHUSU MWANDISHI

Badrane Benlahcene ni Profesa wa mambo ya ustaarabu na falsafa ya historia katika Idara ya Falsafa, Chuo Kikuu cha Batna, Aljeria, na Idara ya Taaluma ya Kiislamu, na Kitivo cha Sanaa, Chuo Kikuu cha Mfalme Feisal, Al-Ahsa, Saudi Arabia. Benlahcene ni mtaalamu aliyebobea katika kazi ya Bennabi ambaye amechapisha makala katika majarida mengi na kuwasilisha mada kuhusu Bennabi na masomo ya ustaarabu katika mikutano mikubwa nchini Aljeria, Moroko, Saudi Arabia na Malayasia

Tovuti: http://drbadrane.com

**Malik Bennabi, msomi** na mwanachuoni maarufu wa Algeria alifanya utafiti wa kuangalia chanzo na suluhisho la kuanguaka Waislamu na sababu ya kuibuka na kufanikiwa utamaduni wa Kimagharibi. Tatizo kubwa, amesema katika nadharia yake ya utafiti kuwa siyo Qur'an au imani ya Kiislamu, bali ni Waislamu wenyewe.

Kitabu hiki kinachambua mbinu aliyotumia Bennabi kutafiti Ustaarabu kupita fani ya nadharia anuai ya kuzichambua nadharia nyingine. Kitabu kinautathimini utafiti huo na kudhihirisha moja ya vipengele vya nadharia hiyo vyenye mvuto muhimu, kwamba Ustaarabu unajengwa na misingi ya ndani na nje inayotokana na jamii yenyewe na taaluma yake.

Kwa misingi ya nadharia hiyo, inapatikana kanuni ya hisabati kuhusu Ustaarabu, kwamba: Ustaarabu ni jumla ya; Watu, Ardhi na Muda, ambapo nafasi ya dini katika Ustaarabu imebainishwa kuwa kichocheo pekee muhimu kitakacho wainua upya Waislamu na kuwarejesha tena kwenye hadhi yao ya awali.

Na kwakuwa watu ndio mhimili wa ustaarabishaji, Waislamu, kama hawajabadili nafsi zao, hawatoweza kuleta mabadiliko yenye manufaa kwa jamii.

London Office
IIIT Books-In-Brief Series

978-1-56564-596-7